Sudan Kusini

Mwongozo wa Mwalimu

# Kiswahili 1

**Kiswahili kwa kidato cha Kwanza (1)** kimeandikwa na wizara ya Elimu na Mafunzo kwa jumla, Ikishirikiana na wataalam wa lugha.

Kitabu hiki kinamwelimisha mwanafunzi kwa mazoezi na vitendo.

**Kila darasa linajumuisha Kitabu cha Mwanafunzi na Mwongozo wa Mwalimu.**

**Kila Kitabu cha mwanafunzi kinakupa:**

- Ufafanuzi mwafaka wa mtaala wa kitaifa.
- Msingi bora katika kiswahili.
- Uwasilishaji na ufafanuzi wa hoja unazotakiwa kujifunza.
- Mazoezi mwafaka yanayoonyesha jinsi Kiswahili Kinaweza kutumika katika mifano halisi maishani.
- Fursa ya ushirikiano kupitia kwa kazi ya vikundi.
- Michoro ya kusisimua.

**Masomo yote katika mfululizo huu wa msingi yalitengenezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mkuu, Jamhuri ya Sudan Kusini.**

**Vitabu vimeundwa kutekeleza somo la shule za msingi,na wakati huo huo kuwawezesha wanafunzi na ujuzi unaofaa katika jamii ya kisasa ya kimataifa**

**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kitabu kitakachopatikana kikiuzwa kwa njia yoyote kitatawaliwa na muuzaji kuchukuliwa hatua za kisheria.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

Sudan Kusini

Mwongozo wa Mwalimu

# Kiswahili 1

## Kidato cha Kwanza



**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

# Jinsi ya kutunza kitabu chako.

## Mambo muhimu ya kuzingatia.

1. Unaombwa kuhakikisha umenawa mikono kabla ya kukitumia kitabu chako.
2. Tumia kalamu ya rangi kuonyesha kazi iliyofanywa.Usikunje karatasi za vitabu.
3. Kitabu kikiharibika,hakikisha kinakarabatiwa kwa haraka.
4. Kuwa mwangalifu wakati unapomwazimu mwenzako kitabu.
5. Tafadhali kiweke kitabu chako mahali pakavu na pasipokuwa na unyevu.
6. Unapokipoteza kitabu chako, mjulishe mwalimu wako.

## Mambo unayokatazwa kufanya.

1. Usiandike ndani au juu ya kitabu chako.
2. Usikate michoro iliyokitabuni.
3. Usirarue kurasa zozote kitabuni.
4. Usikiache kitabu kikiwa kimefunguliwa.
5. Usikiweke kitabu chako kwenye mkoba uliojazwa vitabu zaidi.
6. Usikitumie kitabu chako kujifunika wakati wa mvua.
7. Usikikalie kitabu chako.

Sudan Kusini

KIDATO CHA

1

# Kiswahili

## *Mwongozo wa Mwalimu*

©2018, THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN, MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION. All rights reserved. No part of this book may be reproduced by any means graphic, electronic, mechanical, photocopying, taping, storage and retrieval system without prior written permission of the Copyright Holder. Pictures, illustrations and links to third party websites are provided in good faith, for information and education purposes only.

Ilifadhiliwa na:

Kitabu hiki ni Mali ya Wizara
Kimetadhiliwa na: ya Elimu na Mafunzo.

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

**KITABU HIKI HAKIRUHUSIWI KUUZWA.**

FOREWORD

I am delighted to present to you this Teacher's Guide, which is developed by the Ministry of General Education and Instruction based on the new South Sudan National Curriculum. The National Curriculum is a learner-centered curriculum that aims to meet the needs and aspirations of the new nation. In particular, it aims to develop (a) Good citizens; (b) successful lifelong learners; (c) creative, active and productive individuals; and (d) Environmentally responsible members of our society. This textbook, like many others, has been designed to contribute to achievement of these noble aims. It has been revised thoroughly by our Subject Panels, is deemed to be fit for the purpose and has been recommended to me for approval. Therefore, I hereby grant my approval. This Teacher's Guide shall be used to facilitate learning for learners in all schools of the Republic of South Sudan, except international schools, with effect from 4th February, 2019.

I am deeply grateful to the staff of the Ministry of General Education and Instruction, especially Mr Michael Lopuke Lotyam Longolio, the Undersecretary of the Ministry, the staff of the Curriculum Development Centre, under the supervision of Mr Omot Okony Olok, the Director General for Quality Assurance and Standards, the Subject Panelists, the Curriculum Foundation (UK), under the able leadership of Dr Brian Male, for providing professional guidance throughout the process of the development of National Curriculum, school textbooks and Teachers' Guides for the Republic of South Sudan since 2013. I wish to thank UNICEF South Sudan for managing the project funded by the Global Partnership in Education so well and funding the development of the National Curriculum, the new textbooks and Teachers' Guides. I am equally grateful for the support provided by Mr Tony Calderbank, the former Country Director of the British Council, South Sudan; Sir Richard Arden, Senior Education Advisor of DfID, South Sudan. I thank Longhorn and Mountain Top publishers in Kenya for working closely with the Ministry, the Subject Panels, UNICEF and the Curriculum Foundation UK to write the new textbooks. Finally, I thank the former Ministers of Education, Hon. Joseph Ukel Abango and Hon. Dr John Gai Nyuot Yoh, for supporting me, in my role as the Undersecretary, to lead the Technical Committee to develop and complete the consultations on the new National Curriculum Framework by 29 November 2013.

The Ministry of General Education and Instruction, Republic of South Sudan, is most grateful to all these key stakeholders for their overwhelming support to the design and development of this historic South Sudan National Curriculum. This historic reform in South Sudan's education system is intended to benefit the people of South Sudan, especially the children and youth and the future generations. It shall enhance the quality of education in the country to promote peace, justice, liberty and prosperity for all. I urge all Teachers to put this textbook to good use.

May God bless South Sudan. May He help our Teachers to inspire, educate and transform the lives of all the children and youth of South Sudan.

Deng Deng Hoc Yai, (Hon.)
**Minister of General Education and Instruction, Republic of South Sudan**

# YALIYOMO


Sura ya kwanza 1: Maaamkuzi .......................................................... 1

Sura ya pili 2: Shule yetu ............................................................ 13

Sura ya tatu 3: Uchukuzi .............................................................. 23

Sura ya nne 4 : Mwili na usafi ....................................................... 30

Sura ya tano 5: Nyumbani kwetu ................................................... 38

Sura ya sita 6: Ushirikiano,amani na utulivu ..................................... 45

# Sura ya kwanza 1: Maaamkuzi

**A. Kusikiliza na kuzungumza**

**Somo 1** : Maamkuzi

**Malengo maalum:** Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

-  Kuzungumza akizingatia maamkuzi yafaayo katika miktadha mbalimbali na nyakati tofautitofauti.
-  Kuzungumza kwa mfululizo huku akizingatia matamshi bora na sarufi mwafaka.
-  Kuandika mazungumzo katika muktadha wa shuleni na nyumbani kwa njia inayofaa.
-  Kupambanua msamiati unaotokana na mazingira ya shuleni

**Mawaidha kwa mwalimu**

Mazungumzo na maamkuzi huambatana na mafunzo yanayopewa kipa umbele katika Kiswahili. Sababu ni kuwa, mara nyingi watu huwasiliana kwa njia ya kuzungumza. Nayo mazungumzo haya huathiriwa na mambo mengi kama vile dini, umri, rika, mazingira, mada na utamaduni. Ni vyema mwanafunzi kufahamu na kujizoesha sajili mbalimbali ili aweze kukuza na kutumia msamiati na kaida zifaazo za mazungumzo. Wape wanafunzi nafasi ya kufanya mazoezi ya kuongea darasani huku ukiwaelekeza kuhusu msamiati, matamshi na kanuni nyingine muhimu kulingana na sajili inayohusika. Vilevile, ingefaa uwahimize kutumia Kiswahili nje ya darasa huku wakizingatia msamiati ufaao kulingana na sajili. Pia waelekeze kusoma tamthilia, riwaya na hata magazeti ya Kiswahili na baadaye uwaongoze kujadili matumizi ya lugha yaliyomo.

**Utaratibu**

-  Anza kwa kuwauliza maswali kadha kuhusu maamkuzi na mazungumzo katika muktadha wa darasani na nyumbani.
-  Waagize wawili wao kuja mbele ya darasa na kuamkuana na kuzungumzia suala fulani linalohusu Uislamu au ukristo huku ukiwapa mwongozo kuhusu msamiati ufaao katika muktadha huo.

-  Waongoze kusoma mazungumzo yaliyomo kitabuni. Wachague wawili wawili kusoma huku ukiwaelekeza kuhusu usomaji bora. Hakikisha kuwa wengi wao iwezekanavyo wamepata nafasi ya kusikilizanakuzungumza.
-  Waite wawili wawili kuja mbele ya darasa wakiwa na vitabu vya kusoma na wajaribu kuigiza maamkuzi na mazungumzo hayo kwa ufasaha huku ukiwapa maelekezo.
- Pitieni msamiati na pia mjadili maana za msamiati mwingine wasiouelewa.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo na kuwashauri vilivyo. Tathmini maigizo ya mazungumzo yao na kuhakikisha kuwa yanafuata kanuni zilizozungumziwa hapo juu. Tilia maanani na matamshi ya kila neno. Jambo muhimu hapa ni kutamka kwa ufasaha na ukakamavu. Shirikisha wanafunzi wengi iwezekanavyo.

**Kuandika**

**Somo** : Alfabeti ya Kiswahili

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

-  Kutambua herufi za alfabeti ya kiswahili.
-  Kutambua irabu na konsonanti.
-  Kutofautisha irabu na konsonanti.
-  Kuandika maumbo ya herufi za alfabeti ya Kiswahili kwa usahihi.

**Vifaa**

Kanda za kunasia sauti zenye alfabeti, kadi, chati na mabango ya maumbo ya herufi

**Utaratibu**

-  Waulize kuandika alfabeti yoyote wanayoijua.
-  Dondosha herufi zisizo za kiswahi.

- Waulize kutaja herufi zilizobaki.
- Waelekeze kurejelea kitabu cha mwanafunzi na kutaja herufi ambazo hawakuwa wameziandika.
- Watajie herufi hizo nao wakirudia.
- Wape muda nao wazitaje peke yao.
- Rudia nao pamoja mojamoja huku wakiziandika.
- Wape muda wa kuandika. Pita ukiangalia jinsi wanavyoandika maumbo ya herufi. Hakikisha herufi za juu, kati na chini zinajitokeza sawasawa.
- Kagua wanavyoandika maumbo ya herufi wanapoandika maneno. Hati ya kila mwanafunzi ni muhimu kwa vile itampa ukakamavu.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Lengo la mada hii ni mwanafunzi kujua maumbo ya herufi za alfabeti ya Kiswahili. Ni jukumu la mwalimu kutafuta mbinu mwafaka ili mwanafunzi azijue herufi za alfabeti ya Kiswahili – hata kama ni kufinyanga maumbo ya herufi itafaa, itumie. Gawa alfabeti ya Kiswahili katika makundi mawili: irabu na konsonanti. Baadaye, utaweka herufi hizo pamoja. Tunga wimbo ikiwezekana.

**Tathmini**

- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

1. Irabu za Kiswahili kwampangilio kama: a, e, i, o, u.
2. Konsonanti za Kiswahili kwa mfuatano sahihi ni:
   b, ch, d, dh, f, g, gh, h, j, k, kh, l, m, n, ng’, ny, p, r, s, sh, t, th, v, w, y, z.
3. majibu ya irabu iliyoachwa:
   ____a_____, e, ____i____,____o____ u.

**(Mwalimu, hakiki kazi za wanafunzi walivyoandika.)**

**C. Kusoma**

**Somo I** : Ufahamu – Mawasiliano ya adabu katika familia

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.

- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali yanayotokana naufahamu.
- Kutaja majina ya familia aliyokumbana nayo katika kifungu.
- Kutumia maamkuzi aliyokumbana nayo katika kifungu.
- Kupambanua msamiati unaotokana na mazingira ya nyumbani.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na maamkuzi katika familia, kwa mfano:
  a) Nani kiongozi wa familia?
  b) Babu ni nani?
  c) Shangazi ni nani?
  d) Nani anayestahili kumwamkua mwenzake katika familia?
  e) Salamu zina umuhimu gani?

- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimyakimya.
- Baadaye chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti. Wanafunzi wengi iwezekanavyo, wahusishwe. Kila mwanafunzi asome aya moja.
- Waongoze kujadili majina yanayotumika katika familia kama vile mama,baba,kaka,dada,nyanya,babu na mjukuu.
- Waogoze kutaja maamkuzi na maneno ya adabu na heshima yaliyotumika katika kifungu.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati namaamkuzi pamoja na maneno ya adabu na heshima yaliyotumika.
- Waelekeze wanafunzi kufahamu na kutofautisha maamkizi na maneno ya adabu.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa mashauri yanayofaa.

**a) Majibu ya maswali**

1. Baba alipowaamkua watoto wake walimjibu,“Hatujambo”.
2. Siku hiyo ilikuwa ya umuhimu kwavile ilikuwasiku ya ukumbusho wa babu yao.
3. Sababu ya msimulizi kulia ilikuwa vile babu yake aliaga/alimpoteza babu yake.
4. Mkazamjomba
5. Nduguze baba

**b) Mazungumzo: Nyumbani**

Wanafunzi waigize kwa kutamka maneno kwa ufasaha na kuibua hisia za mahusiano ya babu na mjukuu. Kiimbo na shadda katika matamshi vitiliwe maanani. Hisia ni muhimu katika mazungumzo, maamkuzi na adabu na heshima. Mjukuu lazima azungumze kwa sauti ya unyenyekevu na upole kuliko babu. Salamu zifuatazo hujibiwa aje?

**c)Majibu ya salamu**

1. Shikamoo? – Marahaba!
2. Hujambo? – Sijambo!
3. Mama hajambo? – Hajambo!
4. Juma alikuwa ameenda kwa babu kumsalimia.
5. Maneno**kuachwa na mume** yanamaanisha **kufiwa na mume.**

**d) Maneno ya adabu na heshima katika swali (b)**

hodi, hodi tena, karibu, karibu ndani, karibu kiti ukae, starehehe, asante, pole, kumpa makiwa, aliachwa na nani, aliyefiwa

**e) Chunguza sentensi za wanafunzi. Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno ya adabu kudhihirisha maana. Zingatia maana na sarufi.**

**Somo II** : Ufahamu – Sehemu za nyumbani

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua sehemu mbalimbali za mazingira ya nyumbani.
- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali yanayotokana na ufahamu.
- Kutumia maamkuzi aliyokumbana nayo katika kifungu.
- Kupambanua msamiati unaotokana na mazingira ya nyumbani.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na mazingira ya nyumbani, kwa mfano:
    a) Je, nyumba za mashambani zinafanana na za mijini?
    b) Je, mambo yapi ya kushangaza katika nyumba za mijini?
    c) Je, nyumba za mashambani zina uzuri gani?
    d) Je, ni kupi kuzuri kwa kuishi: mashambani au mjini?
    e) Je, mahali pa kwenda haja panaitwaje?
- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimyakimya.
- Baadaye chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti. Wanafunzi wengi iwezekanavyo, wahusishwe. Kila mwanafunzi asome aya moja.
- Waongoze kujadili majina yanayotumika kama vile msala,sebule, barazani, kizingiti, mtambaa panya, paa, uchaga, kichaga, zizi la ng’ombe, kizimba, na mengine mengi kutegemea na mazingira ya nyumbani.
- Waogoze kutaja msamiati wa mazingira ya nyumbani na maana au umuhimu wake.

- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa mashauri

yanayofaa.

**Majibu**

1. Sebuleni
2. Darini
3. hewa safi, mito safi, misitu na nyumba za kitamaduni
4. Kitanda, godoro, blanketi, shuka, meza ndogo, ndara
5. Hakiki matumizi ya msamiati huo.

**D. Sarufi**

**Somo** : Aina za maneno

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana ya aina za maneno.
- Kutambua aina za maneno katika sentensi
- Kutumia aina mbalimbali za maneno kutunga sentensi.
- Kujibu maswali mbalimbali kuhusiana naaina za maneno.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwakumbusha wanafunzi kuhusu aina za maneno ukitumia maswali ya dodoso kama vile:
  a) Nomino ni nini?
  b) Kitenzi ni nini?
  c) Kiwakilishi ni nini?
  d) Kivumishi ni nini?
  e) Kielezi ni nini?

- Waelekeze kupitia maelezo yaliyomo kitabuni. Waambie wasome matini kuhusu aina za maneno huku ukiwapa mifano na ufafanuzi zaidi. Pia waongoze kutoa mifano ya ziada kuhusu kila aina ya kielezi.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya mazoezi yaliyomo kuhusu aina za maneno kisha usahihishe na kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

**a) Kutaja vitenzi vilivyotumika katika sentensi zifuatazo:**

1. Kaka **amerudi.**
2. Yeye **alimshukuru**sana.
3. Baba **alitusalimia**.
4. Simba **alimkimbiza** mama.
5. Salamu za rafiki yangu **zilinifurahisha.**
6. Maji **yalimumwangikia** babu.

b) Nomino katika aya hiyo ni:

1. dada
2. uji
3. Mama
4. Vikombe
5. mkate
6. siagi
7. baba
8. kiamsha kinywa**.**

**c) Kutunga sentensi**

Mwalimu, hakikisha wanafunzi wanatunga sentensi sahihi wakitumia aina hizo za amaneno.

d) Jioni –kielezi

Mkungu wa ndizi – nomino

Sote – kiwakilishi

Wa – kivumishi

Wifi – nomino

Kuzipanga – kitenzi

Nne – kiwakilishi

Kwa – kihusishi

Tangu - kihusishi

**E. Kuandika**

**Somo I** : Upatanisho wa kisarufi

**Malengo maalum** : Baada ya funzo mwanafunzi aweze:

-  Kufafanua maana ya maneno "upatanisho wa kisarufi".
-  Kubainisha ngeli mbalimbali za Kiswahili kulingana na kigezo cha upatanisho wa kisarufi.
-  Kupatanisha nomino za Kiswahili na maneno mengine yaliyotumika kwenye tungo.
-  Kujibu maswali yaliyomo kwa njia sahihi.

**Vifaa**

Chati yenye ngeli za nomino za Kiswahili kulingana na kigezo cha upatanisho wa kisarufi.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kufikia sasa wanafunzi wameshajifunza mengi kuhusu aina za maneno. Sasa ni wajibu wako kuwafunza ngeli ili upatanisho wa kisarufi uwe na mantiki. Wajue mbona viambishi awali vya vitenzi na vivumishi hubadilika. Zidi kuwapa mawaidha, mazoezi na maelekezo zaidi. Jaribu kutumia vifaa mbalimbali vya kufundishia unapofanya hayo. Vile vile wape nafasi ya kubainisha matumizi ya ngeli mbalimbali kimuktadha hasa kutokana na vitabu vya ziada na vya fasihi. Kumbuka, ngeli ndio msingi wa sarufi, na, kwa hivyo, ni muhimu sana wanafunzi kuzielewa na kuzitumia katika miktadha mbalimbali, sio tu darasani lakini hata nje ya darasa.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu ngeli kama vile:

a) Ngeli ni nini?

b) Ni nini umuhimu wa ngeli katika mawasiliano?

c) Neno chaki limo katika ngeli gani kulingana nautaratibu wa upatanisho wa kisarufi?

d) Taja ngeli mbalimbali za Kiswahili, na kadhalika.

- Waelekeze wanafunzi kusoma maelezo na ufafanuzi uliomo kitabuni. Waweza kuwapa nafasi ya kusoma mmoja mmoja kwa sauti huku ukiwafafanulia zaidi na kuwapa mifano ya ziada. Pia waulize maswali katika kila hatua. Unaweza kuwaagiza kuandika baadhi ya majibu unayowauliza ubaoni ili jambo hili liwe chanzo cha mjadala darasani. Unaweza kuwapa wanafunzi ambao wanatatizika zaidi katika weledi wa funzo hili ufafanuzi zaidi wakiwa mmoja mmoja na hata mazoezi ya ziada. Hakikisha umeyasahihisha na kuwashauri. Pia endelea kuwapa moyo huku ukiwaonyesha kwamba kuelewa ngeli ni jambo rahisi sana mradi tu mtu afahamu kanuni zinazotumika katika kuziratibu.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri.

**Majibu**

a) Kuandika maneno katika wingi

| | |
|---|---|
| 1. mikono | 2. wajukuu |
| 3. wajomba | 4. madarasani |
| 5. marashi | 6. migomba |
| 7. majembe | 8. mabua |
| 9. unga | 10. kalamu |

b) Kuandika sentensi katika wingi

1. Mababu walifika na vigoda mikononi.
2. Walimu wamebeba vitabu vizuri.
3. Wakulima watakuwa na majembe wakienda mashamabani.
4. Mvua ikinyesha msicheze nyanjani.
5. Mahali petu ni pazuri kushinda kwenu.

c) Kuandika sentensi katika umoja

1. Mjeledi uliotumiwa na askaritawala ni hatari.
2. Unga uliomwagika ulichafuka.
3. Ugonjwa huo umeenea mno.
4. Mganga ni mwongo sana.
5. Ua wa boma lake unaporomoka.

*Zoezi la ziada*

Licha ya zoezi hili unaweza kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi kutokana na vitabu mbalimbali vya kusoma hasa riwaya. Unaweza kuwaagiza kuorodhesha matumizi mbalimbali ya nomino katika ukurasa au sura fulani. Pia unaweza kutumia vitabu teule vya fasihi kudondoa matumizi mbalimbali ya ngeli, jambo ambalo laweza kuibusha majadiliano darasani.

**Somo II** : Zoezi la ziada - Insha ya masimulizi

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutumia msamiati wa nyumbani kwa usahihi.
- Kutaja sifa za insha ya masimulizi
- Kuandika insha ya masimulizi vizuri
- Kusimulia kisa kwa ufasaha..

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uandishi wa insha kwa jumla, kwa mfano:
  a) Insha ni nini?
  b) Ni mambo gani yanayofaa kuzingatiwa katika uandishi wa insha?
  c) Insha ya masimuliziina sifa zipi?
- Waelekeze kusoma kimya vifungu katika vitabu, magazeti na majarida kuhusu familia na mazingira.
- Chagua wanafunzi wa kueleza mambo yanayohusu familia na mazingira ya nyumbani. Waelekeze jinsi ya kutumia lugha ya kusimulia kwa kushawishi na

na kuvutia. Wanapozungumza, tilia mkazo kiimbo na shadda ili lugha ivutie na ishawishi kutegemea na jambo analozungumzia.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri zaidi. Hakikisha kuwa wanafunzi wanaandika insha hizi kwa wakati tofautitofauti ili kukuza na kuwaelimisha umuhimu wa mshikamano katika familia kwani familia ndio msingi wa jamii. Hakikisha unasahihisha insha hizo ukiwaelekeza na kuwashauri vilivyo. Hakikisha:

1. Wanafunzi wanaandika insha kwa mtiririko mwafaka.
   Wanatoa hoja kuhusu manufaa ya ushirikiano.
2. Wanafunzi wanatumia msamiati wa ukoo kwa usahihi, adabu na heshima katika familia na mazingira ya nyumbani
3. Wanafunzi matukio mbalimbali kama sherehe za harusi, kubatiza, tohara, upanzi, kukaribisha mgeni, mtu kupata tuzo na nyingine nyingi maadam zinaleta aila pamoja.

# Sura ya pili 2: Shule yetu

## A. Kusikiliza na kuzungumza

**Somo** : Shairi

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua sehemu mbalimbali za mazingira yashuleni
- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kupanua msamiati wa kuamkuana kwake.
- Kujibu maswali kwa usahihi.

**Vifaa**

Michoro na picha kuhusu shuleni, makala mbalimbali kutoka magazetini na majaridani kuhusu shuleni.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kama ilivyo kawaida, siku njema huonekana asubuhi. Ni vyema mwanafunzi kujua umuhimu wa masomo na uzuri wa kwenda shuleni kusoma. Ang'amue mapema elimu ni ufunguo wa maisha na ajizi ni nyumba ya njaa. Kwa hivyo, ni jukumu lako mwalimu kutafuta mbinu mwafaka kumwezesha mwanafunzi kujivunia kwenda shule. Vilevile, ajue masomo ni kuyachangamkia. Njia moja ya kuchangamkia masomo ni kufanya somo la Kiswahili kuvutia kwa namna utakayofunza. Kuwa mcheshi na matamshi yako yawe ya kuvutia. Unapoamkuana, kueleza jambo au kuelekeza na kushauri, fanya Kiswahili kivutie. Shairi likaririwe kwa njia nzuri naya kuvutia. Kiswahili huvutia iwapo matamshi yake ni sahihi na kuibua hisia katika mazungumzo na maamkuzi kwa mwanafunzi ipasavyo. Kwa hivyo, kuwa mwanga wa kuwaelekeza kutamka na kuthihirisha hisia mwafaka. Kwa mfano: kuna tofauti ya hisia baina ya 'makiwa' na 'umeamkaje'. Kuwa kielelezo na mwanga wa matumaini.

**Utaratibu**

- Waelekeze kuhusu somo kwa kuwauliza maswali ya dodoso kama vile:
  - a) Taja umuhimu wa shule.
  - b) Je, kuna tofauti ya mtu aliyesoma na asiyesoma?
  - c) Taja vitu, mahali na watu shuleni?
- Kariri shairi kwa mahadhi kwanza kabla ya wao kufungua kitabu cha mwanafuzi.
- Waulize kuhusu ujumbe katika shairi.
- Wafungue vitabu na ukariri pamoja nao.
- Waache wakariri peke yao.
- Waongoze kurudia kukariri shairi. Tilia mkazo matamshi, shadda na kiimbo
- Waelekeze kuelewa istilahi/msamiati wa ushairi kama: ubeti/beti, mshororo/mishororo, kibwagizo/vibwagizo, mizani, kina/vina, malenga, manju, kukariri, kuimba na kuboronga sarufi.
- Wape muda wajibu maswali. Jadili nao majibu ya maswali darasani kabla ya kuwaruhusu kuandika majibu yenyewe.

**Tathmini**

Waongoze kujibu maswali yaliyomo kisha uyasahihishe na kuwashauri zaidi.

**Majibu**

1. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema kuwa kijana aache uvivu na aende shuleni asome kwani elimu itamfaa maishani.
2. Kulingana na ubeti wa pili, mtu akikosa kusoma atakosa nguo, mlo na sukari.
3. Kulingana na ubeti wa tatu mtu akisoma anaweza kuwa serahangi,mtaalamuau mtafiti.
4. Ujumbe unaojitokeza katika shairi hili ni kwamba elimu ni muhimu katika maisha ya mwanafunzi.
5. Maisha ni magumu na ya kusumbua. Mtu anafaa kuwa mwenye akili na

maarifa aliyopata shuleni atapata tabu. Vijana waende shuleni wasome sana na waache uvivu. (Waelekeze kuandika katika lugha ya nathari)

**B. Kusoma**

**Somo** : Ufahamu – Shuleni

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake wa shuleni na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali yanayotokana na kifungu cha ufahamu kwa usahihi.

**Vifaa**

Picha, michoro na mabango kuhusu mazingira ya shuleni

**Mawaidha kwa mwalimu**

Ndio mwanzo mkoko unaalika maua. Wanafunzi wameanza kujua msamiatai wa shuleni katika Kiswahili. Hakikisha kuwa umewapa nafasi ya kuongea bila upingamizi wowote kuhusu mazingira hasa baada ya kusoma kifungu hiki. Unaweza kuwapa nafasi ya kushiriki katika mazungumzo kati yao na vidato vingine hapo shuleni au kati yao na wafanyakazi shuleni. Hali hii itawahamasisha mno kuhusu msamiati na ukakamavu na kujivunia Kiswahili zaidi na kuelewa mengi kuhusu mazingira ya shuleni. Kwa mfano, unaweza kuwa na mijadala au midahalo, mazungumzo, maigizo na mashairi.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uharibifu wa mazingira kama vile:

a) Je, umekalia nini?
b) Je, unaona nini?
c) Je, unaweza kumsalimu jirani yako?
d) Je, unaweza kutaja maneno kumi ya darasani?
e) Je, nje ya darasa kuna nini?.

- Soma aya ya kwanza kwa sauti huku ukizingatia usomaji mwafaka ili uwe kielelezo kwa wanafunzi wako.
- Waagize kusoma kwa sauti huku ukiwaelekeza kuhusu usomaji ufaao. Kila mwanafunzi anaweza kusoma aya moja. Hakikisha kuwa wengi wao wamepata nafasi ya kusoma hasa wale walio na shida za usomaji. Kwa mfano, iwapo kuna mwanafunzi ambaye hugugumiza anaposoma, mpe nafasi zaidi ya kushiriki katika usomaji na uhakikishe kuwa hachekwi au kufanyiwa mzaha na yeyote darasani eti kwa vile ana shida ya kusoma. Ni bora uwafunze wanafunzi wako umuhimu wa kuheshimiana na kuthaminiana.
- Baada ya kusoma waongoze kujadili msamiati wasioufahamu pamoja namasuala mazito yaliyojitokeza. Unaweza kuwaelekeza kutunga sentensi wakitumia baadhi ya msamiati ili kuthibitisha maana yake.

**Tathmini**

- Waulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa kwa mdomo wala si kwa kuandika.
- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri zaidi.

Mwalimu, tilia maanani matamshi ya kila mwanafunzi. Waelekeze kutamka maneno ipasavyo.

**Majibu**

1. Wanafunzi waandike msamiati wa shuleni uliotajwa katika kifungu hiki.
    - shuleni
    - kipindi
    - somo la Kiswahili

- mwalimu
- darasani
- wanafunzi
- mwalimu
- vitabu vya kusoma
- vitabu vya kuandikia
- alitufunza
- kutuuliza maswali
- niliinua mkono
- tafadhali mwalimu
- kipindicha kupumzika.
- Mwalimu Mkuu
- kuruka
- kukimbia
- mchezo wa kujificha.
- alimwomba msamaha
- pole,nisamehe
- nimekusamehe

2. "Hamjambo wanfunzi?"–"Hatujambo mwalimu!"
3. Wanafunzi walitoa vitabu vya kusoma na kuandikia.
4. Maneno yanayoonyesha kuwa wanafunzi wamefunzwa msamiati wa adabu ni, tafadhali,nisaidie,pole naomba msamaha,nimekusamehe.
5. Mwalimu mkuu

(Mwalimu, hakiki majibu.)

**Majibu**

1. Chumba cha kusomea ni**darasa.**
2. Anayefunza huitwa**mwalimu**.
3. **Mwanafunzi**ni yule anayefunzwa .
4. Nakala ambayo mwanafunzi huandikia zoezi ni**kitabu**.

## C. Sarufi

**Somo I** : Umoja na wingi wa nomino

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kufafanua maana ya nomino.
- Kutaja nomino mbalimbali.
- Kutumia ngeli za nominokwa usahihi.
- Kuandika nomino katika umoja na wingi.
- Kuandika sentensi akizingatia upatanisgho wa kisarufi.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Upatanisho wa kisarufi ni ujuzi muhimu kwa mwanafunzi na mtumiaji yeyote wa lugha ya Kiswahili. Sababu ni kuwa mwanafunzi asipomudu jinsi ya kupatanisha maneno katika tungo, hataweza kumudu sarufi ya Kiswahili ambayo ndiyo msingi wa lugha. Kutokana na sababu hii, inafaa sana mwanafunzi apewe ufafanuzi na mazoezi ya kutosha kuhusu upatanisho wa kisarufi. Msingi wa upatanisho wa kisarufi ni kujua umoja na wingi ndipo atajua maumbo ya nomino yanavyobadilika.

**Utaratibu**

- Andika nomino ubaoni kisha uwaambie wanafunzi wazisahihishe;

  kwa mfano:

  a) Matoto
  b) mavitabu
  c) fijiko
  d) vidawati
  e) manyumba

- Waongoze wanafunzi kupitia maelezo yaliyomo kitabuni pamoja na jedwali.
- Wanapoyapitia wape ufafanuzi zaidi pamoja na mifano ya ziada na uwaagize kutoa mifano ya ziada.

**Tathmini**

Lengo la mada hii ni wanafunzi kujua upatanisho wa sarufi. Ngeli ni muhimu katika upatanisho huu. Kwa hivyo, wanafunzi kujua umoja na wingi wa nomino utawawezesha kujua viambishingeli kwa haraka. Sahihisha kazi hiyo ukiwashauri

na kuwaelekeza ipasavyo.

**Majibu**

a) Wanafunzi waandike umoja na wingi wa nomino.

| | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| 1. | mwalimu | **walimu** |
| 2. | **mwanafunzi** | wanafunzi |
| 3. | bendera | **bendera** |
| 4. | **kalamu** | kalamu |
| 5. | mwalimu mkuu | w**alimu wakuu** |
| 6. | mazingira | mazingira |
| 7. | wembe | nyembe |
| 8. | bawabu | mabawabu |
| 9. | ua | nyua |
| 10. | sekritari | sekritari |

b) Wanafunzi waandike sentensi katika wingi.

1. Walimu walikuja.
2. Walimu wakuu wanatufunza.
3. Vitabu vilisahihishwa.
4. Masomo yalifunzwa vizuri
5. Kalamu zilipotea

**Somo II** : Uakifishaji

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutaja alama za kuakifisha mbalimbali.
- Kueleza matumizi ya alama mbalimbali za kuakifisha.
- Kutumia alama mbalimbali za kuakifisha kwa njia inayofaa.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kuakifisha ni stadi ya kimsingi kwa mwanafunzi na mtumiaji yeyote wa lugha. Sababu ni kuwa uakifishaji bora huhitajika kila mara mtu anapoandika maandishi

ya aina mbalimbali iwe ni barua, insha, muhtasari, hadithi fupi na mambo mengine. Vilevile, wakati wa kusoma, kila alama ya kuakifisha ina uamilifu wake. Kutokana na umuhimu huu wa alama za kuakifisha, ni bora wanafunzi wazidi kupewa mafunzo na mazoezi mwafaka kuhusiana na alama za kuakifisha. Zaidi ya mafunzo katika sarufi, unaweza kupata mazoezi zaidi katika vitabu vya fasihi, magazeti, majarida na kadhalika. Unaweza kuwapa mazoezi ya kusoma vifungu na kutilia maanani alama za kuakifisha zilizotumika.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu funzo hili; kwa mfano:
    a) Ni nini maana ya uakifishaji?
    b) Ni nini umuhimu wa kuakifisha?
    c) Taja alama tatu za kuakifisha na ueleze matumizi yake.
    d) Alama ya kikomo hutumika katika mazingira gani, na kadhalika.
- Waongoze kupitia maelezo yaliyomo huku ukiwafafanulia zaidi na kuwapa mifano mwafaka. Washirikishe kwa kuwaagiza watoe mifano zaidi. Mara kwa mara unaweza kuandika sentensi ubaoni na kuwataka kutia alama mwafaka.
- Wape mazoezi kuhusu kila alama kisha uyasahihishe na kuwashauri.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo mwishoni mwa maelezo hayo kisha uzunguke darasani ukiwapa mashauri.

**Majibu**

**a) Wanafunzi waandike sentensi kwa kuweka alama iliyofungiwa kuakifisha.**

1. Mwanafunzi aliingia darasani**?**(swali)
2. Mwalimu alisoma maswali**,**majibu na kuyaandika.(koma)
3. Bendera ya shule ilipeperushwa**?**(swali)
4. Kitabu cha Kiswahili kinasomwa**.**(kituo)
5. Darasa**,** viti na meza zimepaguswa.(koma)

b) **Kuakifisha kifungu.**

Heshima ni kitu cha maana mno.Wazee kwa vijana, wavulana kwa wasichana, wanafunzi kwa walimu, sote ni binadamu,Iwe uko shuleni ama nyumbani ni

vyema kuishi na kushirikiana na wenzako vyema. Hili hutokana na heshima

ambayo huleta amani na utangamano katika jamii. Jamii isiyo na heshima miongoni mwa watu wake huwa haina ushirikiano mwema.

(Mwalimu, hakiki majibu.)

**Somo 3** : Kuandika - Silabi za Kiswahili.
**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutamka silabi za Kiswahili kwa usahihi.
- Kuandika silabi za Kiswahili kwa usahihi.
- Kuunganisha silabi na kupata neno.
- Kutamka maneno kwa ufasaha.
- Kupambanua/kuainisha silabi za Kiswahili.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Waelekeze wanafunzi kutamka silabi kwa ufasaha.
Wanafunzi watamke sauti kwa ufasaha. Wasikilize na kuwarekebisha matamshi na kuwashauri ipasavyo. Waelekeze kuelewa miundo ya silabi na aina zeke. Wape mifano na wafanye mazoezi. Unaweza kuwaongeza mazoezi mengine mengi ili kuwazoesha kuelewa mada kwa kina.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na silabi za Kiswahili, kwa mfano:
    a) Kiswahili kina irabu ngapi?
    b) Unaweza kutamka baadhi ya konsonanti za Kiswahili.
    c) Silabi za Kiswahili zina muundo gani?
    d) Maneno ya Kiswahili yana muundo gani wa silabi?
    e) Kiswahili kina konsonanti ngapi?

- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye silabi na kuwaambia wasome kwa sauti.
- Baadaye chagua mmoja mmoja asome kwa sauti.
- Waongoze kujadili silabi na kujadili zinazotatiza kutamka.
- Waelekeze kutunga maneno wakitumia silabi hizo.

- Mwalimu, sasa tamka kwa ufasaha silabi za Kiswahili. Ziandike ubaoni kwahati nadhifu. Tamka nao kisha uwaambie watamke ukiwaelekeza na kuwashauri.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa mashauri

yanayofaa.

1. Waongoze kutamka silabi kwa ufasaha. Sikiliza matamshi na kurekebisha punde matamshi mabaya yatokeapo.
2. Waongoze wanafunzi kutamka silabi kwa ufasaha.
3. Waongoze kuainisha silabi za Kiswahili.
4. Kagua maendelezo ya maneno na kuwarekebisha wanafunzi na kuwashauri ipasavyo.

## Sura ya tatu 3: Uchukuzi

### A. Kusikiliza na kuzungumza

**Somo** : Kukariri shairi

**Malengo maalum** : Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

- Kutaja sifa za mashairi.
- Kuchangamkia mashairi.
- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kutaja hatua za kuimarisha usalama katika usafiri.

**Majibu**

Majina ya michoro ya vyombo vya usafiri:

1. Meli
2. Gari moshi
3. Tuk Tuk
4. Baiskeli
5. Ndege
6. Pikipiki
7. Gari
8. Lori
9. Basi
10. Jahazi

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kuna haja ya wanafunzi kuchangamkia Kiswahili. Njia moja ni kupitia mashairi. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Waeleze na kuwaonyesha arudhi: mizani, vina na muwalana maudhui ya shairi kwa jumla. Ikiwezekana, watungie shairi fupi la kuwatolea mfano. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe. Mbinu hiyo itarahisisha matamshi yao na kufanya

wapende kuzungumza na kusikiliza Kiswahili. Waambie mtunzi wa mashairi anaitwa malenga.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwakariria shairi lako mwenyewe.
- Waulize kama wanajua shairi. Kama wapo kadhaa wanaokubali waulize:
  a) Kutaja kwa jumla, sifa za mashairi.
  b) Ni vipengele gani muhimu unavyopaswa kuzingatia katika kukariri shairi?
  c) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?
- Waelekeze kwa shairi lililo kitabuni. Wakaririe.
- Waulize kurudia kukariri baada yako.
- Kariri nyote kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri. Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaousu mawasiliano na uchukuzi.
- Ni kupitia kukariri, watarudia msamiati wa uchukuzi na kuzoea kuutaja bila woga.
- Waelekeze katika maudhui ambapo shairi hili lazungumzia kuhusu usalama katika uchukuzi.

**Tathmini**

- Waelekeze wanafunzi katika kujibu maswali waliyoagizwa. Kwanza, wajibu kwa kujadiliana darasani. Waelekeze. Waruhusu kuandika madaftarini. Unaposahihisha ona kuwa silabi na maneno yameandikwa kuzingatia sarufi wala si kuboronga jinsi ilivyo katika shairi.
- Mwanafunzi atumie lugha ya kinathari kujibu maswali huku akizingatia ujumbe.

Kabla ya kumaliza kipindi, ni muhimu kuwakumbusha istilahi za ushairi walizosoma. Hilo litawawezesha kuona ushairi kuwa sehemu muhimu ya lugha na mawasiliano. Kariri nao tena shairi kwa mahadhi ya kuvutia kuwachangamsha na

kuwaelekeza ili uwaache wakiwa wanakariri na kuzungumzia shairi na Kiswahili kwa jumla. Ni kama kuwaacha na asali kinywani.

**Majibu**

1. Mshairi anaomba Mungu awalinde wasafiri safarini.
2. Vyombo vinne vya usafiri vinavyoweza kupata ajali nimeli, matwana, magari, na feri.
3. Katika ubeti wa 5 na 6, mshairi anawaomba manahodha, marubani, madereva namakondakta wadumishe usalama katika uchukuzi.

## B. Kusoma

**Somo** : Ufahamu – Kuponea chupuchupu

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutamka na kuandika maneno kwa usahihi.
- Aeleze anachotaka katika maeneo ya uchukuzi kwa ufasaha
- Awasiliane na watu katika maeneo ya uchukuzi kwa usahihi na ufasaha.
- Kujibu maswali katika maeneo ya uchukuzi kwa usahihi.

**Vifaa**

Picha, michoro na mabango kuhusu vyombo vya uchukuzi, kwa mfano, matatu, pikipiki, tuktuk, meli, parachute, poritangi, gari la moshi, treni, jahazi, motaboti, baiskeli na lori.

**Majibu:**

Vyombo vya usafiri vilivyotajwa katika taarifa ni:

1. Basi,
2. Pikipiki
3. Motokaa

4. Gari la moshi.
5. Lori
6. Mkokoteni
7. Meli
8. Jahazi
9. Ngalawa
10. Dau
11. Mashua
12. Ndege

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uchukuzi, kama vile:
  a) Je, umewahi kusafiri?
  b) Je, ulitumia chombo gani?
  c) Je, ni vizuri kusafiri kwa gari linalosafiri kwa kasi mno?
  d) Je, vyombo vya usafiri vya angani, majini, ardhini ni vipi?
  e) Ukiwa waziri wa uchukuzi utachukua hatua ipi kwanza?
- Soma aya ya kwanza kwa sauti huku ukizingatia usomaji mwafaka ili uwe kielelezo kwa wanafunzi wako.
- Chagua mmoja mmoja wakisoma kila mmoja aya moja. Waagize kusoma kwa sauti huku ukiwaelekeza kuhusu kumaka maneno kwa ufasaha. Kila mwanafunzi anaweza kusoma aya moja; wasome wakipokezana. Ni bora uwafunze wanafunzi wako umuhimu wa kuheshimiana na kuthaminiana.
- Baada ya kusoma waongoze kutaja na kujadili msamiati wasioufahamu pamoja na masuala mazito yaliyojitokeza. Unaweza kuwaelekeza kutunga sentensi wakitumia baadhi ya msamiati ili kuthibitisha maana yake.

**Tathmini**

- Waulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa kwa mdomo wala si kwa kuandika.
- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri zaidi.

## C. Sarufi

**Somo** : Kujieleza

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua majina ya vyombovya usafiri.
- Kubainisha vyombo vya majini, angani na ardhini.
- Kuwasiliana katika maeneo ya usafiri kwa ufasaha.
- Kuandika mambo anayotaka kuhusu uchukuzi.
- Kujibu maswali yaliyomo kwa njia sahihi.

**Vifaa**

Chatina mbango yenye vyombo vya usarifi

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kufikia sasa wanafunzi wameshajifunza mengi kuhusu uchukuzi. Wajibu wako ni kuzidi kuwapa mawaidha, mazoezi na maelekezo zaidi. Jaribu kutumia vifaa mbalimbali vya kufundishia unapofanya hivyo. Vilevile, wape nafasi ya kuzuru maeneo ya uchukuzi wakajionee na kushuhudia shughuli za huko. Hakikisha unawapa msingi bora wakujieleza bila woga kwani kama tujuavyo huo ndio mwanzo na msingi wa kujua. Kwa hivyo,ni muhimu sana wanafunzi kuelewa shughuli za uchukuzi na msamiati wake na kuzitumia katika miktadha mbalimbali, sio tu darasani lakini hata nje ya darasa.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe nakuwashauri ipasavyo. Kumbuka: wanafunzi wanafaa waweze kutumia msamiati
wa usafiri kwa usahihi kwenye maeneno ya usafiri. Waweze kujieleza na kusema wanachotaka bila utata wowote.

**Majibu**

a) Kuchagua jibu sahihi kutoka kwa majibu yaliyofungiwa.

   1. Chombo cha usafiri kinachopitia majini ni _______. (**meli,**gari)

2. ________ni Kubebwa na chombo cha uchukuzi.**(Kusafiri,**kukimbia)
3. ________ ni chombo kikubwa sana cha uchukuzi.(baiskeli,**Ndege)**
4. mtu anayeendesha gari huitwa________.(abiria,**dereva)**
5. Malipo anayolipa mtu anaposafiri ni ________.(nauli, abiria)

b) Kujaza nafasi kwa msamiati sahihi wa usafiri.

Usafiriau **uchukuzi**ni njia ambazo hutumika kwa kusafiria.Hutumia vyombo kama vile b**aiskeli, matatu,ndege**na**meli**.Kuna vyombo vya usafiri ambavyo hutumia barabara,kama vile **matatu,baiskeli,** gari na lori.Vingine husafiria hewani kama vile **ndege**.Meli husafiria majini.Mtu anayesafiri huitwa msafiri au **abiria.**Msafiri anapaswa kuulizia wakati au saa ambapo chombo cha usafiri kitaondoka ili asiachwe.Pia aulize mwelekeo au kule ambako chombo hicho kinaenda ili asipotee.Mtu anapoabiri chombo cha usafiri analipa kondakta pesa zinazoitwa **nauli.**

## D. Kuandika

**Somo** : Insha masimulizi

**Malengo maalum:** Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

-  Kusimulia kisa kuhusu safari aliyowahi kusafiri.
-  Kutaja sifa za insha ya masimulizi.
-  Kutumia msamiati wa uchukuzi kwa usahihi.
-  Kutunga insha kuhusu ajali barabarani.

**Vifaa**

Kanda za kunasia sauti zenye maneno ya uchukuzi, makala kutoka katika magazeti, majarida na vitabu

**Utaratibu**

-  Wakumbushe sifa za insha ya maelezo na mjadala kwa maswali ya dodoso kama vile:
    a) Insha ni nini?
    b) Kusimulia ni kufanya nini?

c) Masimulizi huandikwa katika wakati gani?

d) Masimulizi huwa na sifa zipi?

e) Insha huwa na urefu gani? na kadhalika.

- Ikiwezekana wasikilize kanda zenye masimulizi kuhusu sehemu za uchukuzi.
- Waongoze kusoma masimulizi mbalimbali na mifano ya insha za masimulizi. Washirikishe kwa kuwauliza maswali mbalimbali katika kila hatua.

**Tathmini**

- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

1. **Maneno na sentensi**

   Lengo ni mwanafunzi kuweza kutunga maneno na kuyatumia katika sentensi kwa usahihi. Vilevile, kuandika maneno na sentensi kwa mwandiko mzuri unaosomeka na kueleweka.

2. **Insha**

   Mwanafunzi abuni kisa juu ya safari aliosafiri.Sahihisha insha hiyo ukiwashauri na kuwaelekeza ipasavyo..

3. Wanafunzi washirikiane kuandika kisa juu ya umuhimu wa vyombo vya uchukuzi. Wape vidokezonauwasahihishie kazi ukiwashauri na kuwaelekeza ipasavyo.

# Sura ya nne 4 : Mwili na usafi

## A. Kusikiliza na kuzungumza

**Zoezi: Ambatanisha sehemu ya mwili na kazi yake.**

kuona



kutembea





kukula



kusikia



kugusa



kunusa

**Somo** : Kukariri shairi

**Malengo maalum** : Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

- Kutaja sifa za mashairi.
- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kusikiliza kwa makini
- Kukuza msamiati wake.
- Kuchangamkia mashairi.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kuna haja ya wanafunzi kutanzukiwa kikamilifu na kusikiliza kwa makini na kutamka maneno kwa usahihi. Vile tulivyosema hapo awali, buni mbinu mbalimbali za kukuza matamshi hata ikiwa ni nyimbo, mijadala, mazungumzo na hotuba. Kukuza kipawa cha kuzungumza hadharani na kutamka kwa usahihi na ufasahasilabi na maneno ni jambo muhimu sana. Hili huwapa wanafunzi ujasiri mno. Vilevile, kutilia mkazo, shadda, kiimbo na toni. Kwa hivyo, mashairi na nyimbo, kama Sanaa, vitawawezesha kuchangamkia Kiswahili na hiyo itakuwa hatua nzuri katika kufunza na kuwahamasisha na somo na lugha hii. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Hili litawezekana endapo wewe mwenyewe utakuwa unakariri na kutamka maneno kwa ufasaha mno. Zingatia shadda na kiimbo. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe. Mbinu hiyo itarahisisha matamshi yao na kufanya wapende kuzungumza na kusikiliza Kiswahili.

Kwa hivyo, Sehemu hiini ya kuwakuza wanafunzi katika kutamka na kusikiliza.Lengo ni kuwa, wanafunzi waweze kutamka maneno kwa usahihi na kusikiliza wanapozungumziwa. Kuwakumbusha istilahi za ushairi na arudhi za ushairi. Itakuwa vyema kuwaeleza kuwa shairi hili ni la arudhi aina ya tarbia. Fafanua zaidi kuhusu aina za mashairi.

**Utaratibu**

- Anza kukariri shairi ulilotunga mwenyewe.
- Kisha waulize maswali ya kuwadodosa kama vile:

  a) Nani atakariri shairi?
  b) Nani atatutajia sifa za shairi?
  c) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?
- Huku mkirejelea shairi lililo katika Kitabu cha Mwanafunzi, wakaririe kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri. Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaousu usafi na jinsi ya kujitunza.

**Majibu**

**Majina ya sehemu za mwili.**

1. Sikio
2. Jicho
3. Shingo
4. Bega
5. Kifua
6. mkono
7. Kiuno
8. vidole
9. goti
10. mguu

**Shairi.**

1. Askari, nesi, jamaa, madaktari, wanafunzi
2. Mshairi anawalaumu manesi kwa sababu wanauliwa wakijua.
3. Shairi hili linaonya juu ya adhabu mtu atapata kwa kukosa kushughulikia afya yake.

## B. Kusoma

**Somo** : Ufahamu – Mwili na usafi

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kusoma kifungu kwa ufasaha
- Kujadiliana na wenzake kuhusu ujumbe katika kifungu.
- Kujibu maswali kwa usahihi.
- Kutaja aina mbalimbali za usafi wa mwili na wa jumla.

**Vifaa**

Picha, michoro na mabango kuhusu sehemu za mwili, chati ya majina ya sehemu za mwili

**Mawaidha kwa mwalimu**

Mwanafunzi aweze kutamka maneno yaliyotumika katika kifungu kwa usahihi. Vilevile, atumie msamiati wa usafi kwa usahihi na kuzingatia usafi wake na wa mazingira yake. Aweze kujibu maswali ya kifungu kwa usahihi. Ni wajibu wa mwanafunzi kuzingatia elimu anayoipata na kuitekeleza. Tafuta mbinu inayoweza kuwafanya wajivunie usafi wao na wamazingira yao bila kujali mila na utamaduni.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu usafi wa mwili, kama vile:
  a) Je, tunafaa kupiga mswaki mara ngapi kwa siku?
  b) Je, tunafaa kuoga mara ngapi kwa siku?
  c) Je, umewahi kumwona mtu na matongo machoni?
  d) Uchafu unaokwama menoni unaitwaje?
- Soma aya ya kwanza kwa sauti huku ukizingatia usomaji mwafaka ili uwe kielelezo kwa wanafunzi wako.

- Waagize kusoma kwa sauti huku ukiwakosoa na kuwaelekeza kuhusu usomaji ufaao. Kila mwanafunzi anaweza kusoma aya moja. Hakikisha kuwa wengi wao wamepata nafasi ya kusoma hasa wale walio na shida za usomaji. Kwa mfano, iwapo kuna mwanafunzi ambaye hugugumiza anaposoma, mpe nafasi zaidi ya kushiriki katika usomaji na uhakikishe kuwa hachekwi au kufanyiwa mzaha na yeyote darasani eti kwa vile ana shida ya kusoma. Ni bora uwafunze wanafunzi wako umuhimu wa kuheshimiana na kuthaminiana.
- Baada ya kusoma waongoze kujadili msamiati wasioufahamu pamoja na masuala mazito yaliyojitokeza. Unaweza kuwaelekeza kutunga sentensi wakitumia baadhi ya msamiati ili kuthibitisha maana yake.

**Tathmini**

- Waulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa kwa mdomo wala si kwa kuandika.
- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri zaidi.

**Majibu**

1. Njia za kuupumzisha mwili ni kulala,kula chakula cha afya na kuoga.
2. Kulingana na kifungu, mtu asiyeoga ananuka vibaya, anavamiwa na wadudu,nzi wanamfuata,hatari ya kupatwa na magonjwa.
3. Kufua, kuoga, kunawa, kupiga mswaki, kutoogea/kufulia mtoni
4. i)nta -uchafu wa masikioni
   ii)matongo-uchafu wa macho

## C. Sarufi

**Somo** : Maneno yenye sauti zinazorudiwa

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua sauti mbalimbali zilizorudiwa katika maneno.
- Kubainisha sauti zilizorudiwa katika maneno.
- Kutambua silabi zilizozorudiwa katika maneno.
- Kuandika nomino katika umoja na wingi.
- Kujibu maswali yaliyomo kwa njia sahihi.

**Vifaa**

Kadi, chatina mabango zenye sauti za Kiswahili, silabi na maneno

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kufikia sasa wanafunzi wameshajifunza mengi kuhusu sauti. Wajibu wako ni kuzidi kuwapa mawaidha, mazoezi na maelekezo zaidi. Jaribu kutumia vifaa mbalimbali vya kufundishia unapofanya hayo. Vilevile, wape nafasi ya kutunga maneno mengi wakitumia sauti chache, kama nne au sita. Kwa mbinu hiyo, wanafunzi watazielewa sauti za Kiswahili na kuzitumia kuunda maneno mengi katika miktadha mbalimbali, sio tu darasani lakini hata nje ya darasa.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu nomino kama vile:
  a) Nomino ni nini?
  b) Ni nini umuhimu wa nomino katika mawasiliano?
  c) Nini wingi wa nomino 'mwanafunzi'
  d) Nomino 'mwanafunzi' imo katika ngeli gani kulingana utaratibu wa upatanisho wa kisarufi?
  e) Taja ngeli mbalimbali za Kiswahili, na kadhalika.
- Waelekeze wanafunzi kusoma maelezo na ufafanuzi uliomo kitabuni. Waweza kuwapa nafasi ya kusoma mmoja mmoja kwa sauti huku ukiwafafanulia zaidi na kuwapa mifano ya ziada. Pia waulize maswali katika kila hatua. Unaweza kuwaagiza kuandika baadhi ya majibu unayowauliza ubaoni ili jambo hili liwe chanzo cha mjadala darasani. Unaweza kuwapa wanafunzi ambao wanatatizika zaidi katika weledi wa funzo hili ufafanuzi zaidi wakiwa mmoja mmoja na hata mazoezi ya ziada.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe nakuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

a) Mwanafunzi azingatie maneno aliyopewa na kutunga sentensi sahihi.

1. Ni muhimu kudumisha **usafi** wa mwili ili kuyaepuka magonjwa.
2. Tunapaswa **kupiga mswaki**, kila baada ya kula.
3. Kunywa **maji safi** hudumisha afya ya mwili.
4. Ni lazima kukitumia **choo kisafi** ili kuzuia viini vinavyo sababisha magonjwa.
5. Wakati **tunapoziosha nguo** zetu, tunapaswa kutumia sabuni.

b) Maneno kutokana na silabi hizo kwa kurudiarudia ni:

1. popo
2. kaka
3. baba
4. nyanya
5. gogo
6. yaya
7. chacha
8. lulu
9. tingatinga
10. pikipiki

c) Kujaza sentensi kwa silabi za kurudiwa

1. Dereva anaendesha tinga**tinga**.
2. Meno yake yana meta**meta**.
3. mtoto anakula pi**pi.**
4. Pa**pa** anaishi baharini.
5. Nilimtembelea nya**nya**.

## D. Kuandika

**Somo** : Insha ya maelezo

**Malengo maalum:** Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza ya insha ya maelezo.
- Kutaja sifa za insha ya maelezo.
- Kuandika insha ya maelezo.
- Kujieleza kwa usahihi.

**Vifaa**

Kanda za kunasia sauti zenye maelezo, makala kutoka katika magazeti, majarida na vitabu.

**Utaratibu**

- Wakumbushe sifa za insha ya maelezo kwa maswali ya dodoso kama vile:
  - f) Maelezo ni nini?
  - g) Hutolewa kwa madhumuni gani?
  - h) Je, kuoga kuna umuhimu gani?
  - i) Insha huwa na urefu gani? na kadhalika.
- Ikiwezekana wachezee kanda zenye maelezo kuhusu jambo Fulani kuhusu usafikisha mzichambue.
- Waongoze kusoma maelezo katika vitabu na magazeti huku ukiwafafanulia zaidi. Washirikishe kwa kuwauliza maswali mbalimbali katika kila hatua.

**Tathmini**

- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

1. Wanafunzi waandike vifaa vya lazima ambavyo mtu anapaswa kutumia kwa kuoga kama vile sabuni, karai, kitambaa cha kuoga, maji safi, jiwe lakusugua kisigino.
2. Wanafunzi waandike kisa juu ya umuhimu wa kuoga mwili kila siku. Mwalimu asahihishe insha.

# Sura ya tano 5: Nyumbani kwetu

## A. Kusikiliza na kuzungumza

**Somo** : Kukariri shairi

**Malengo maalum** : Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

- Kutaja sifa za mashairi.
- Kuchangamkia mashairi.
- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kusikiliza kwa makini
- Kukuza msamiati wake.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kufikia sasa, wanafunzi wanajua kutamka kwa usahihi. Kuza ukakamavu wao kwa kuimba shairi huru hili. Waeleze tofauti kati ya mashairi huru na arudhi.

Vile tulivyosema hapo awali, buni mbinu mbalimbali za kukuza matamshi hata ikiwa ni nyimbo, mijadala, mazungumzo na hotuba. Kukuza kipawa cha kuzungumza hadharani na kutamka kwa usahihi maneno na silabi ni jambo muhimu sana. Hili huwapa wanafunzi ujasiri mno. Vilevile, kutilia mkazo, shadda, kiimbo na toni.

Kwa hivyo, mashairi na nyimbo kama sanaa vitawawezesha kuchangamkia Kiswahili na hiyo itakuwa hatua nzuri katika kufunza na kuwahamasisha na lugha hii. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Hili litawezekana endapo wewe mwenyewe utakuwa unakariri na kutamka maneno kwa ufasaha mno. Zingatia shadda na kiimbo. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe. Mbinu hiyo itarahisisha matamshi yao na kufanya wapende kuzungumza na kusikiliza Kiswahili.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza maswali ya kuwadodosa kama vile:
  a) Nani atakariri shairi?
  b) Nani atatutajia sifa za shairi?
  c) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?
- Wape muda waeleze tofauti ya muundo wa mashairi yaliyotangulia na hili. Kisha wakariri kwa sauti. Tilia mkazo mahadhi yao ukiwaelekeza na kuwashauri ipasavyo.
- Huku mkirejelea shairi lililo katika Kitabu cha Mwanafunzi, wakaririe kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri. Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaohusu nyumbani na kuutumia kutunga sentensi sahihi.

**Majibu**

1. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema nyumba inajengwa kwa matofali, boriti au chuma, kuta na miti nau mbao.
2. Shughuli zinazofanywa nyumbani ni kufagia, kuosha, kupanga na kusafisha mazingira.
3. Mambo mawili yanayokuzwa nyumbani ni upendo na adabu.
4. Nyumbani ni nyumbani kwa sababu familia ipo na kuna umoja.

**B. picha.**

Waelekeze wanafunzi wajadiliane kuhusu shughuli zinazodhihirika kwenye picha.wape mwelekeo ufaao.

**C. Kusoma**

**Somo** : Ufahamu: Mazungumzo – Marafiki wawili

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutamka maneno kwa ufasaha.
- Aeleze anachotaka kwa ufasaha.
- Awasiliane na watu usahihi na ufasaha.

- Kujibu maswalikwa usahihi.

**Vifaa**

Picha, michoro na mabango kuhusu nyumbani na shughuli za nyumbani, chati na kadi za msamiati wa nyumbani.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Lengo la mazungumzo haya ni ushirikiano. Kidole kimoja hakivunji chawa. Uhusiano mwema nyumbani pamoja na majirani ni muhimu. Vivyo hivyo ilivyo darsani na shuleni.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uchukuzi, kama vile:
  a) Mahali chakula hupikiwa huitwaje?
  b) Je, mtu hulala katika chumba gani?
  c) Je, ni vizuri kuogea barazani?
  d) Je, unajua vyombo vyombo vya sebuleni?
  e) Sehemu ya ndani ya juu ya nyumba huitwaje?
  f) Nani kiongozi wa nyumbani
- Soma aya ya kwanza kwa sauti huku ukizingatia usomaji mwafaka ili uwe kielelezo kwa wanafunzi wako.
- Waagize kusoma kwa sauti huku ukiwakosoa na kuwaelekeza kuhusu usomaji ufaao. Kila mwanafunzi anaweza kusoma aya moja. Hakikisha kuwa wengi wao wamepata nafasi ya kusoma hasa wale walio na shida za usomaji.
- Baada ya kusoma waongoze kujadili msamiati wasioufahamu pamoja na masuala mazito yaliyojitokeza. Unaweza kuwaelekeza kutunga sentensi wakitumia baadhi ya msamiati ili kuthibitisha maana yake.

**Tathmini**

- Waulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa kwa mdomo wala si kwa kuandika.
- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri zaidi.

**Majibu**

1. Katika kifungu hiki kwakina Asha ni Mashariki/mashambani.
2. Nyumba ya kina Asha ina vyumba vinne.
3. Chumba cha maankuli hutumiwa na watu kukaa wakipumzika na wakati wa kula.

**Picha: vyombo na vifaa vya nyumbani.**

**1.** Sahani na vikombe.
2. Vijiko, vijiko vya uma na kisu.
3. mwiko
4. sufuria
5. jiko
6. meza

## B. Sarufi

**Somo** : Ukanushaji wa vitenzi

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua vitenzi katika sentensi.
- Kuandika vitenzi.
- Kutaja nyakati katika vitenzi.
- Kukanusha vitenzi.
- Kujibu maswali kwa usahihi.

**Vifaa**

Chati na mabango yenye vitenzi, nyakati na ukanusho.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kufikia sasa wanafunzi wameshajifunza mengi kuhusu vitenzi. Wajibu wako ni kuzidi kuwapa mazoezi na maelekezo zaidi. Jaribu kutumia vifaa mbalimbali vya

kufundishia unapofanya hayo. Vilevile, wape nafasi ya kubainisha viambishi vya nyakati na viwakilishi vya nafsi kwa vile huchangia katika mabadiliko ya umbo la neon katika ukanusho.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu vitenzi kama vile:
  a) Kitenzi ni nini?
  b) Kuna nyakati ngapi?
  c) Kukanusha ni kufanya nini?
- Wataje vitenzi ukiviandika ubaoni.
- Waelekeze kutambua nyakati katika baadhi ya vitenzi ulivyoviandika ubaoni.
- Waelekeze kutambua viwakilishi vya nafsi kwenye vitenzi vilivyo ubaoni
- Waelekeze wanafunzi kusoma maelezo na ufafanuzi uliomo kitabuni. Waweza kuwapa nafasi ya kusoma mmoja mmoja kwa sauti huku ukiwapa nafasi ya kutambua: nyakati na nafsi
- Sasa, waelekeze kukanusha vitenzi. Fafanulia zaidi na kuwapa mifano ya ziada. Pia waulize maswali katika kila hatua.
- Waelekeze kutofautisha kukanusha na kinyume. Dhana hizo mbili hukanganya. Unaweza kuwapa wanafunzi ambao wanatatizika zaidi katika weledi wa funzo hili ufafanuzi zaidi wakiwa mmoja mmoja na hata mazoezi ya ziada.

**Tathmini**

Hakikisha umeyasahihisha na kuwashauri ipasavyo.Pia endelea kuwapa moyo huku ukiwaonyesha mradi tu mtu afahamu kanuni zinazotumika katika kukanusha.

**Majibu**

**a) Wakati uliotumika katika sentensi.**

Wanafunzi waandike majibu sahihi kwa kutumia nyakati. Mwalimu, hakiki kazi za wanafunzi ukiwashauri na kuwaelekeza ipasavyo.

**Mfano.**Nitaenda dukani. (wakati ujao)

1. Yaya amemlaza mtoto.(hali timilifu)
2. Nchi yetu inapendeza.(wakati uliopo)
3. Jirani yao alifuga kuku.(wakati uliopita )
4. Mito yote ilifurika.(wakati uliopita)
5. Sinia zote zinaoshwa.(wakati uliopo)
6. Ufagio mpya utanunuliwa.(wakati ujao)
7. Mama anamlaki mgeni.(wakati uliopo)
8. Mwalimu anaingia darasani kila siku.(wakati ulopo)
9. Watamkaribisha mwenzao leo.(wakati ujao)
10. Mlimtembelea babu yenu?(wakati ulopita)

**b) Kukanusha vitenzi katika sentensi.**

Wanafunzi wakanushe vitenzi katika sentensi kwa usahihi.Mwalimu,hakiki majibu.

1. Mama hapiki chakula.
2. Hamtamwimbia nyanya wimbo.
3. Kuku wetu hakutaga mayai.
4. Situmii maji kuosha choo chetu.
5. Nyumba yetu haijajengwa upya.
6. Mfanyakazi wao hataenda shambani.
7. Chumba cha kulala hakina vitanda viwili.
8. Chakula cha kikwetu hakipendezi.
9. Hawatakunywa maziwa yote.
10. Hatukuchemshia maji ya kunywa jikoni.

## D. Kuandika

**Somo** : Kutunga sentensi

**Malengo maalum:** Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza sehemu za sentensi

- Kutaja uamilifu wa maneno katika sentenzi.
- Kutunga sentensi za aina mbalimbali: kama sahili, ambatani na changamano.
- Kuakifisha sentensi kwa usahihi.

**Vifaa**

Kadi, chati na mabango ya maneno, sehemu za sentensi na sentensi

**Utaratibu**

- Wakumbushe aina za maneno kwa maswali dodoso kama vile:
  a) Taja nomino.
  b) Taja kitenzi.
  c) Je, kuna sentensi ya kitenzi pekee?
  d) Je, unaweza kutumia nomino mbili katika sentensi?
  e) Nani anaweza kutumia kiunganishi katika sentensi?
- Waelekeze kupanga maneno kuunda sentensi. Anza na sentensi sahi, ambatano kisha changamano.
- Waelekeze kufahamu mtendaji na kitendo katika sentensi.
- Washirikishe kwa kuwauliza maswali mbalimbali katika kila hatua. Wape muda waandike sentensi zao. Kagua kisha wape muda wa kufanya zoezi kitabuni.

**Tathmini**

Sahihisha sentensi za wanafunzi. Tilia maanani vitenzi vilivyokanushwa. Hakikisha wamezingatia sarufi na maana.

**Kwa mfano,**

1. Juma hataenda mtoni.
2. Rehema hatajenga nyumba.
3. Abdalla hatakuwa askari.
4. Suleimani hatakuwa kandawala.
5. Mariamu hatakuwa mwanariadha.

## Sura ya sita 6: Ushirikiano,amani na utulivu

### A. Kusikiliza na kuzungumza

**Funzo** : Kukariri shairi – Uchaguzi wanukia

**Malengo maalum** : Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

- Kutaja sifa za shairi.
- Kuchangamkia mashairi.
- Kutamka maneno kwa usahihi na ufasaha.
- Kusikiliza kwa makini
- Kutumia msamiati kutunga sentensi kwa usahihi
- Kujibu maswali kwa usahihi.

### Mawaidha kwa mwalimu

Katika sehemu hii, tutilie maanani matamshi ya maneno. Wanafunzi wapokezane kukariri shairi hilo kwa mahadhi yanayostahili.

Jambo ni kushirikiana na kushauriana kuhusu matamshi bila kuona kinyongo wala ubaya. Waelekeze wanafunzi kujadili kuhusu picha katika kitabu na kuhusu ujumbe katika shairi.

Vile tulivyosema hapo awali, buni mbinu mbalimbali za kukuza matamshi hata ikiwa ni nyimbo, mijadala, mazungumzo na hotuba. Kukuza kipawa cha kuzungumza hadharani na kutamka kwa usahihi maneno na silabi ni jambo muhimu sana. Hili huwapa wanafunzi ujasiri mno.

Vilevile, kutilia mkazo, shadda, kiimbo na toni. Kwa hivyo, mashairi na nyimbo kama sanaa vitawawezesha kuchangamkia Kiswahili na hiyo itakuwa hatua nzuri katika kufunza na kuwahamasisha na lugha hii. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Hili litawezekana endapo wewe mwenyewe utakuwa unakariri na kutamka maneno kwa ufasaha mno. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza maswali ya kuwadodosa kama vile:
  - a) Nani atakariri shairi?
  - b) Nani atatutajia sifa za shairi?
  - c) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?
  - d) Je, shairi lililo katika kitabu ni la aina gani?
- Huku mkirejelea shairi lililo katika Kitabu cha Mwanafunzi, wakaririe kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri. Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaohusu ushirikiano, amani na utulivu. Waelekeze kuutumia kutunga sentensi sahihi.

**Tathmini**

Waelekeze kutamka kwa usahihi. Sahihisha na kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

1. Mshairi analalamikia wabunge wanaotumiamaneno yasiyo navitendo.Wabunge wanaotafuta kuchaguliwa tu kwa sababu ya mshahara.
2. Mshairi anasema atampa kura yake anayemjali.
3. Ujumbe wa shairi nikuwa wananchi wanapaswa kuchagua kiongozi atakayewafaa.

## B. Kusoma

**Somo** : Ufahamu – Ushirikiano

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Aeleze ujumbe wa kifungu kwa ufasaha.
- Ashirikiane na wenzake katika shughuli za shuleni, nyumbani na za jamii kwa jumla.

- Kujua umuhimu wa kushirikiana.
- Kujibu maswali katika maeneo ya uchukuzi kwa usahihi.

**Vifaa**

Picha, michoro na mabango kuhusu ushirikiano, chati za msamiati wa utaifa na ushirikiano

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uchukuzi, kama vile:
  a) Je, mzalendo ni nani?
  b) Je, Amani ni nini?
  c) Je, umoja una umuhimu gani?
  d) Je, vyombo vya dola vinachangia vipi kuleta ushirikiano?
- Waagize kusoma kwa sauti huku ukiwakosoa na kuwaelekeza kuhusu usomaji ufaao. Kila mwanafunzi anaweza kusoma aya moja. Hakikisha kuwa wengi wao wamepata nafasi ya kusoma hasa wale walio na shida za usomaji. Kwa mfano, iwapo kuna mwanafunzi ambaye hugugumiza anaposoma, mpe nafasi zaidi ya kushiriki katika usomaji na uhakikishe kuwa hachekwi au kufanyiwa mzaha na yeyote darasani eti kwa vile ana shida ya kusoma. Ni bora uwafunze wanafunzi wako umuhimu wa kuheshimiana na kuthaminiana.
- Baada ya kusoma waongoze kujadili msamiati wasioufahamu pamoja na masuala mazito yaliyojitokeza. Unaweza kuwaelekeza kutunga sentensi wakitumia baadhi ya msamiati ili kuthibitisha maana yake.

**Tathmini**

- Waulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa kwa mdomo wala si kwa kuandika.
- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri zaidi.

**Majibu**

1. Kulingana na kifungu ushirikiano ni hali ya kujitolea na kuishi vyema na

wengine.

2. Knachoudhi msimulizi juu ya mashabiki wa mpira ni kwamba wanashangilia timu za kigeni na hata wakati mwingine mashabiki wa timu pinzani wanaweza pigana. Wanawafahamu wachezaji wote wa timu hizo ilhali hata pengine wengine wao hawatapata fursa ya kuonana nao maishani. Mashabiki hao hao hawajui timu za nchi yao.
3. Ushirikianao unawafaidi wanafunzi shuleni kwa kusoma pamoja na kupita mitihani yao.
4. Faida za amani katika makazi ya watu kulingana na kifungu ni kuwa watu wataacha kufuga mbwa,kuunda milango ya chuma wala nyumba kuwa na silaha. Mtu akibisha mlango, atafunguliwa bila kuuliza ni nani.
5. Hakiki majibu ya wanafunzi kuhusu njia za nne za kutumia vyombo vya habari kuleta utangamano.

## C. Sarufi

**Somo** : Kutunga sentensi

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

-  Kutambua aina za maneno katika sentensi.
-  Kutambua uamilifu wa maneno katika sentensi.
-  Kutunga sentensi za aina mbalimbali.
-  Kuakifisha sentensi kwa usahihi.

**Vifaa**

Chati na mabango yenye aina za maneno, sentensi na uamilifu wa maneno katika sentensi

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kufikia sasa wanafunzi wameshajifunza mengi kuhusu sentensi. Wajibu wako ni kuzidi kuwapa mawaidha, mazoezi na maelekezo zaidi. Jaribu kutumia vifaa mbalimbali vya kufundishia unapofanya hayo. Vilevile, wape nafasi ya

kubainisha matumizi ya maneno mbalimbali kimuktadha hasa kutokana na vitabu vya ziada. Kujua uamilifu na viambajengo vya sentensi utawapa msingi mwafaka.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu nomino kama vile:
  a) Nomino ni nini?
  b) Umuhimu wa nomino katika sentensi ni upi?
  c) Kitenzi ni nini?
  d) Umuhimu wa kitenzi katika sentensi ni upi?
- Andika maneno yaliyoparaganywa ubaoni ukiwachagua wayapange kuunda sentensi.
- Waelekeze wanafunzi kutunga sentensi wakitumia maneno utakayowapa. Chagua wanafunzi wakisoma sentensi walizotunga.
- Walekeze wanafunzi wawiliwawili kutunga sentensi: sahili, ambatani na changamani. Wachague wakisoma darasani na kujadiliana mpangilio na uamilifu wa maneno katika sentensi hizo. Pia waulize maswali kuhusu aina za maneno na uamilifu wake. Unaweza kuwapa wanafunzi ambao wanatatizika zaidi katika weledi wa funzo hili ufafanuzi zaidi wakiwa mmoja mmoja na hata mazoezi ya ziada.

**Tathmini**

Hakikisha umeyasahihisha na kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

Wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno waliyopewa. Mwalimu, hakiki sentensi za wanafunzi kwa kuzingatia: miundo, uamilifu wa maneno hayo na sarufi pamoja na maana za sentensi.

## D. Kuandika

**FunzoI** : Insha

**Malengo maalum:** Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza matukio yanayotukia katika nchi yake.
- Kutumia msamiati wa utaifa na ushirikiano.
- Kutunga sentensi kwa usahihi.
- Kuandika taarifa ya matukio kutoka maeneo mbalimbali.

**Vifaa**

Magazeti, majarida, michoro, picha na vitabu

**Utaratibu**

- Wakumbushe msamiati wa ushirikiano kwa maswali ya dodoso kama vile:
  a) Mzalendoni nani?
  b) Ushirikiano una manufaa gani?
  c) Taarifa ni nini?
  d) Je, umewahi kusikia taarifa ya matukio kutoka sehemu mbalimbali? na kadhalika.
- Ikiwezekana wachezee kanda zenye taarifa za matukio mbalimbali kisha mzichambue.
- Waongoze kusoma makala kuhusu matukio mbalimbali katika magazeti na majarida. Washirikishe kwa kuwauliza maswali mbalimbali katika kila hatua.

**Tathmini**

- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

Mwalimu, waongoze wanafunzi kusoma magazeti na kuandika ujumbe wa kitaifa unaojitokeza humo.

**Somo II** : Matumizi ya kamusi

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kujua umuhimu wa kamusi.
- Kutumia kamusi.

**Vifaa**

Chati za maneno, michoro, picha na vitabu

**Utaratibu**

- Wakumbushe msamiati wa ushirikiano kwa maswali ya dodoso kama vile:
  a) Mzalendo ni nani?
  b) Ushirikiano una manufaa gani?
  c) Taifa ni nini?
- Wachezee kanda zenye taarifa za matukio ya ushirikiano na utaifa wakiandika msamiati wanaokumbana nao katika kanda hiyo

- Waulize wakutajie msamiati huo ukiuandika ubaoni.
- Waelekeze kutafuta maana ya msamiati huo kwenye kamusi

**Tathmini**

- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

Waongoze wanafunzi kutumia kamusi kufahamu jinsi ya kutafuta maana za maneno kwenye kamusi.